

Utangulizi;

Afya ni ukamilifu wa binadamu kimwili, kiakili na kijamii na kutokuwa na maradhi. Namba 100,000 ina thamani lakini ukiondoa tarakimu ya kwanza ambayo ni 1, namba nzima itapoteza thamani. Tarakimu 1 hapa inawakilisha afya na sifuri zilizobaki zinawakilisha mambo mengine katika maisha kama utajiri, umaarufu, heshima na kadharika. Kama huna afya bora mambo mengine yote huwezi kuyafurahia. Pale ambapo afya za watu hutetereka, wanahitajika wahudumu wa afya kuziweka sawa. Mbali na madaktari na wauguzi ambao ndio wahudumu wa afya wanaofahamika zaidi kuna wahudumu wengine wengi wanaotoa mchango katika kuhakikisha afya za watu zinakaa sawa.



Una ndoto ya kuwa muhudumu wa afya?

Kazi unayoipenda utaifanya kwa ubora, itakupatia mafanikio wewe na jamii inayokuzunguka. Maisha ni vita na kila mtu kapewa siraha itakayomsaidia kushinda vita hii. Siraha hii ni kipaji. Kumbe jambo la msingi ni kujitafuta una kipaji gani. Kazi unayoipenda na kuifanya vizuri tofauti na wengine ndio kipaji ulichojaliwa. Kama ambavyo siraha inatakiwa iboreshwe ili iweze kufaa, kipaji vilevile kinatakiwa kunolewa na ndio maana tunahitaji kwenda shule.

Kumbe ni vizuri uende shule ukijua mapema unakwenda kutafuta nini. Kusoma ni safari, safari hii itakuwa ya mafanikio kama ukijua unaelekea wapi ili uweze kufanya maandalizi ya uhakika. Bahati mbaya muongozo unaouhitaji ili kufikia ndoto yako haufundishwi shuleni. Kama ndoto yako ni ni kuwa muhudumu wa afya, kitabu hiki ndio muongozo wako;

- Kitakusaidia kugundua kama una kipaji na aiba (personality) ya kuhudumu katika afya,
- Kitakusaidia kuzifahamu kwa undani fani mbalimbali za afya ili ujipime utafaa katika fani ipi. Sio kila muhudumu wa afya ni daktari! Kuna taaluma kadha wa kadha za afya na hakuna taaluma iliyo chini ya nyingine bali zote hufanya kazi kwa kutegemeana.
- Kitakusaidia kujua vigezo vinavyohitajika ili kusomea fani mbalimbali za afya katika ngazi mbalimbali za elimu.
- Kitakusaidia kuyatambua mambo unayoyajua kinyume na yalivyo 'myths' juu ya fani za afya.
- Kitakusaidia kujua ni mambo gani uyafanye ili uweze kushinda changamoto zitakazokuzuia usiifikie fani ya ndoto yako, mfano mbinu za kujisomea, kufanya mitihani, kupata ada na kadharika.

**'HATUWEZI KUWA
TUNAVYOTAKA KAMA
TUTABAKI TULIVYO'-
MAX DERE**